**102/3**
**KARATASI YA 3**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

---

1. **MAJIBU YA SHAIRI**

(a) Nafsineni ni mwananchi/raia/mzalendo/mtetezi wa haki za binadamu/za wanyonge.

(b) (i) Tabdila – Kuleta urari wa vina mfano: usitatanizwe, wanaturararuwa.

(ii) Inkisari – Kuleta urari mizani mfano: aso.

(iii) Utohozi – Hi kuleta urari wa vina na mizani mfano: noleji.

(c) (i) Sakarani – Shairi ni mseto wa bahari kadha mfano tathmina, utatu, ukaraguni n.k.

(ii) Kikwamba neno longa linaanzia na kurudiwa kila ubeti.

(iii) Ukaraguni – Vina vya ukwapi na utao vinabadilika kila ubeti.

(iv) Mathnawi – Shairi limegawika vipande viwili kila mshororo.

(v) Kikai – Mizani katika utao ni michache (6) ilhali. Mizani ya ukwapi ni mingi (8).

(vi) Sabilia – Halina pambio bali lina kituo.

(d) (i) Anafora – huu ni urudiaji/uradidi neno longa imerudiwarudiwa.

(ii) Usambamba wa kiusawe – neno longa lina maana sawa na nena, sema, zungumza, ongea, kuli, tamka na ambayo yametumiwa kwenye shairi.

(iii) Usambamba wa kifahiwa/dhamira – mtunzi anadhamiria kusisitiza haja ya kuwaumbua na kuwasuta wabunge walafi na wenye kuzua balaa.

(iv) Tabaini - Si uasi si tenge si noma.
- Si kiwara si medani

(v) Jazanda – Mabubu – Wenye kujitia hamnazo
- Kishindo cha funo – tishio hafifu/tishio la nyamarero

(e) Toni – ghadhabu/hasira

(f) Adhidadi – pole/taratibu

(g) Afwaji – kaumu/halaiki/umati wa watu

<u>2. Nguu za Jadi</u>

<u>Majibu</u>

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- Haya ni maneno ya Ngoswe
- Anamweleza Mashauri.
- Walikuwa nyumbani kwa Ngoswe kwenye mtaa wa Majuu
- Ngoswe alikuwa akimliwaza Mashauri baada ya kumfumania babake na mchumba wake Cheiya.

(4x1=4)

b) Fafanua maana ya kitamathali kwenye kauli iliyopigiwa mstari. (alama 2)

- Watu kuwatendea wenzao unyama/kuwadhulumu/kuwanyima haki/kuwafanyia maonevu. Mfano sagili kumnyakua mchumba wa mwanaye Mashauri.

(1x2=2)

c) Onyesha jinsi unyama wa msemaji kwenye dondoo ulivyoathiri wengine kwenye jamii.(alama 6)

- Ngoswe kufuja kodi ya majumba ya babake hivyo kumnyima mapato
- Ngoswe kukusanya ushuru wa mashamba ya babake na kujiwekea kiasi kisichojulikana hivyo kumhini babake kipato.
- Ngoswe kuwa na marafiki aliowaathiri vibaya waliokataa shule na kuishi kama wafalme kwenye makasri ya wazazi wao
- Ngoswe alikuwa farisi wa biashara haramu ya kulangua dawa za kulevya iliyosemekana kupigwa marufuku. Kwa kuwa alikuwa mwana wa mtemi, wakuu serikalini walishidwa kumchulia hatua.
- Ngoswe kuwa na mtandao wa kulangua dawa za kulevya zilizosambazwa hata na maafisa wa gerezani wakisaidiana na mahabusu hivyo kuathiri utendakazi wa maafisa hao.
- Ngoswe kuwauzia wanafunzi wa shule na vyuo dawa haramu, dawa hizi ziliwaharibu wakaishia kuwa mazube, wengine wakaacha shule na kuwa wazururaji mjini.
- Ngoswe kuendesha biashara haramu iliyoendelea kuimarika na kuharibu vijana na wengine kupoteza maisha yao.
- Ngoswe kuwekeza pesa alizopata kwenye majumba ya starehe na anasa- baadhi ya vilabu vikawa madanguro yaliyowameza vigoli usiku na kuwatapika asubuhi.
- Ngoswe alikuwa mkware- alitumia pesa zake kustarehesha na kuwabadilisha warembo wa mji kila uchao. Aliwafanya wasichana wengi kuwa wazinifu kwa kutumia pesa kama chambo cha kuwanasa

(6x1=6)

d) Kando na msemaji wa dondoo hili, kuna wahusika wengine wanaoendeleza utovu wa maadilikatika jamii. Thibitisha. (alama 10)

- Sihaba kuhusiana kimapenzi na Sagilu ili apate kuchuma pesa kutoka kwake.
- Sagili alikuwa na mazoea ya kuwanyang’anya wanaume wengine wake zao.
- Nanzia anakuwa na uhusiano wa kimapenzi na Sagilu. Matokeo yake ni kuzaliwa kwa Ngoswe.
- Sihaba ana majunba ya danguro anakowatumikisha wasichana wadogo katika biashara hiyo haramu.
- Mrima kuwa na uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa- Mangwasha aliweza kupata barua ya mmoja wa wapenzi wa pambeni wa mumewe.
- Cheiya anamsaliti mchumnba wake mashauri kwa kuhusiana kimapenzi na babake Mashauri.
- Mrima anashiriki ulevi na kutelekeza jukumu la malezi ya wanao.

- Walezi walikosa adabu wakati walijisaidia njiani bila kuwajali wapiti njia.
- Sagili anauza bidhaa za magendo na malori yanayosafirisha bidhaa hizo yanapokamatwa anatoa hongo ili yaachiliwe.
- Mbwashu anashirikiana na viongozi wa nchi kuagiza bidhaa ghushi ambazo hazilipiwi ushuru.
- Sagilu anamhonga Mrima ili asimamie kampeni za Mtemi na pia aharibu kampeni za Mwamba za kuwania kiti cha ubunge cha Matango
- Sagilu aliyauza maziwa yaliyoharibika na kuwaathiri watoto kwa kutapika na kuendesha.
- Mtemi Lesulia kutoa ajira kwa mapendeleo- watu wasio na maarifa wanaajiriwa kwa misingi ya kikabila licha ya kuwepo kwa vijan wengi waliohitimu katika taaluma mbalimbali.
- Mrima kumdhalilisha mkewe kwa kumwambia anaweza kuona wanawake wengi tena wakti wowote bila ushauri wake. (Hoja 10x1=10)

3. Riwaya ya Nguu Za Jadi ni kioo cha nchi za Africa. Fafanua. (alama 20)

- **Ukabila – kuna ubaguzi wa kikabila katika riwaya Watu wa kabila la Waketwa walibaguliwa na kuchukiwa na wakule. Waketwa walizingiziwa kuwa chanzo cha misiba yao, maradhi sugu, ukame, njaa na majanga kama mafuriko.**
- **Tamaa – Matajiri wengi waliongozwa na tamaa ya mali ardhi n.k Waketwa walifurushwa makwao kwa kuchomewa makazi yao ili watu kama Mbwashu na Nanzia wainyakue.**
- **Dhuluma – Kuna uonevu riwayani ; mfano mtaa mzima wa Matango ulichomwa na kuwaacha wakazi wa majengo bila makao vijana walibeba mikebe iliofuka harufu ya petroli.**
- **Ufisadi – kuna wizi wa mali ya umma katika mashirika ya umma au serikari. Pia kuna utumiaji ovyo wa mali ya umma mf sagilu aliwahonga watu ambao walimshinda kwa maarifa ya maisha.**
- **Usherati – Baadhi ya wakeketwa ilisemekana kuwa waliuza wake zao kwa wakuu ili wapate ajira Sagilu aliwabadirisha wanawake kama nguo, pia alimtamani Mangwasha lakini hakumpata.**
- **Ubinafsi – Sagilu ni mbinafsi kwani alitaka afanikiwe peke yake katika biashara. Hivyo aliwapangia njama walioshinda ili kuwafilisisha.**
- **Uongozi mbaya – Viongozi walio mamlakani wanatumia nafasi walizopewa vibaya mfano, viongozi wakule walikuwa wenye majivuno, kiburi na ubaguzi. Vyeo vingi uongozini na kazini vilipewa wakule nao waketwa wakaachiwa Zile kazi duni.**
- **Usaliti – vioingozi wengi wanawasaliti wananchi mfano, viongozi ndio wanaopanga kuwafurusha maskini (waketwa) kwa kuwachomea makazi yao**
- **Umaskini – Umaskini umekithiri hasa katika jamii ya Waketwa mfano Mangwasha anabadilishwa kuwa maskini na ghasia huko Matango, kwa kuchomewa kila kitu.**
- **Ushirikina – Mangwasha alifikiria kuwa mume wake alizugwa na ndipo akakubali kusuhubiana na Sagilu, mtu aliyekuwa adui wa familia ya Waketwa. Haelewi alikuja kukubali pesa za Sagilu vipi.**

- **Uozo katika jamii – kuna uozo wa kila aina katika riwaya, kwa mfano viongozi wanatumia vyeo vyao kutekeleza maovu kama vile, wizi wa mali ya umma, kutoa hongo kushiriki mapenzi kiholela kuendeleza biashara haramu nk.**
- **Ukatili – kuwachomea makazi waketwa ni ukatili.**
- **Ubaguzi wa kijinsia – wanawake wanabaguliwa na kudharauliwa. Chifu mshabaha anamdharau Mangwasha. Hatimaye anamfuta kazi.**
- **Unafiki – Watu wengi katika riwaya wanajifanya wema ilhali ni waovu. Mbwashu anajifanya mwema kwa Lesulia lakini anaposhindwa uchaguzi anamtoroka kwa kwenda ulaya kujificha aibu**
- **Uwongo – Katika riwaya – watu wengine niwaongo mfano, mwanamke aliyefika na kifurushi arusini alidanganya kuwa maarusi walikuwa jamaa zake ili akubaliwe kuwafikia. Nia yake ilikuwa kuwalipua.**

**(**zozote 10 x2)

Mwalimu akadirie hoja za mwanafunzi

**4. Si neno mama! (Kimya.) Hakuna kizuri kijacho kwa urahisi. Mazuri hutoka mbali na wakati mwingine yana hadithi za kutisha.**

**(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)**

*(i) Msemaji ni Sara*

*(ii) Msemewa ni Neema.*

*(iii) Walikuwa kijijini nyumbani kwa kina Neema*

*(iv) Ni baada ya Neema kumweleza Sara kuwa alikuwa amejitolea maisha yake yote ili wapate mema. Hata hivyo, matokeo yake yalikuwa ugonjwa.* *4 x 1 = 4*

**(b) Bainisha mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)**

*(i) Nidaa/ siyahi – si neno mama!*

*(ii) Tashihisi – mazuri hutoka mbali* *2 x 2 = 4*

**(c) Fafanua sifa za msemaji. (alama 6)**

*Msemaji ni Sara*

***(i)*** *Ni mtamaduni/mhafidhina. Sara anakubaliana na utamaduni usiomruhusu yeye kulala kwa Neema. Anawaambia Asna na Neema kuwa utamaduni ulikuwa na mahali pake.*

***(ii)*** *Mlezi mwema – Sara anawalea Asna, Neema na Salome vyema. Kwa mfano anahakikisha kuwa wamepata cha kula kwa kuwapikia mchicha uliochemshwa kwa chumvi na sima baridi.*

***(iii)****Amewajibika – Sara anashirikiana na Yona kumsomesha Neema. Aidha, afya yake ilipokuwa nzuri alishughulikia majukumu yake kama kumpikia mumewe.*

***(iv)*** *Mvumilivu – Sara anastahimili matatizo anayokumbana nayo katika ndoa kama kupigwa na mumewe. Aidha, anavumilia kusemwa na watu kwa kuchelewa kupata watoto.*

***(v)*** *Mwenye mlahaka mzuri – Sara alikuwa na uhusiano mzuri na Dina hivyo anapomtumia salamu aende amsaidie kupika, Dina anafika kumsaidia Sara.*

***(vi)*** *Mshauri mwema – Sara anamshauri Neema kuwa, wanandoa hawafai kushindana kwa kuwa wao ni kama wachezaji wa timu moja.*

***(vii)*** *Mcha Mungu – Sara anatoa shukrani kwa Mungu kwa kuwa alimpa watoto: Neema, Asna na Salome.*

***(viii)*** *Mwenye hekima/busara – Neema anatambua kuwa Sara alikuwa na hekima kutokana na ushauri aliompa.*

***(ix)****Sara ni jasiri – Kiwa anasema kuwa alimwona Sara akitoka kliniki na licha ya unyonge wake alionekana kuwa jasiri.*

***(x)*** *Ni mwenye furaha – Kiwa anasema kuwa kila alipokutana na Sara uso wake ulikuwa umejaa tabasamu.*

***(xi)****Sara ni muungwana – Dina anamtaja Sara kama mmoja katika watu waungwana duniani.*

*6 x 1 = 6*

**(d) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 6)**

*(i) Kubainisha wakati wa matukio – jioni, nyumbani kwao Neema.*

*(ii) Kubainisha mahali pa tendo – nyumbani kwao Neema.*

*(iii)Kutambua sifa za wahusika – kwa mfano, Sara amewajibika kwa kuwa anajitolea kuhakikisha kuwa wanawe walikuwa wamepata mema.*

*(iv) Kubainisha maudhui – kwa mfano mabadiliko – safari za jiji zilikuwa zimebadilika na hazikuwa zikibughudhi kama zamani.*

*(v) Kukuza dhamira ya mtunzi. Mandhari haya yanaonesha madhara ya ulevi. Ulevi unamfanya Yona kutelekeza majukumu yake kwa mfano kufunga kuku na mbuzi mapema ili kwenda kukutana na wazee wenzake.*

*(vi) Kuendeleza ploti – kwa mfano, tunaelezwa kuwa Yona humsaidia Sara wakati mwingine katika kazi za jikoni.*

*(vii) Kubainisha mgogoro*

*(viii) Kutambua wahusika*

Ndiyo ni mgonjwa lakini mume ambaye ni mwanamume kweli hangoji kuelezwa kinafanyika nini."

**5. (a)(i) Bainisha maudhui yanayojitokeza katika dondoo. (alama 1)**

*Ubabedume/ taasubi ya kiume* *1 x 1 = 1*

**(ii) Onyesha jinsi maudhui uliyotaja katika (i) yalivyoshughulikiwa katika tamthilia ya Bembea ya Maisha. (alama 9)**

*(i) <u>Shoka la ugumbwa kumwangukia Sara zaidi.</u> Sara na Yona walipoitwa wagumba kwa kutozaa watoto, Dina anasema kuwa shoka la ugumba lilimwangukia Sara zaidi kuliko Yona.*

*(ii) <u>Mtoto wa kiume ndiye anayerithi mali ya wazazi wake</u>. Yona na Sara wanapopata watoto wa kike pekee, watu walianza kujiuliza ni nani angerithi ardhi ya Yona.*

*(iii) Watu wanamtaka Yona aoe mwanamke mwingine kwa sababu kwa maoni yao Sara alikuwa ameshindwa kumzalia Yona mtoto wa kiume.*

*(iv) Yona anamwuliza Sara sababu ya kutomwandalia chakula ilhali alijua kuwa Sara alikuwa mgonjwa.*

*(v) Yona hamsaidii Sara kupika chakula anapokuwa mgonjwa. Inamlazimu Sara kutuma salamu kwa Dina aende kumsaidia kupika chakula.*

*(vi) Sara anasema kuwa dunia ikijua kuwa Yona anamsaidia mkewe itasemwa kuwa, anashusha hadhi yake.*

*(vii) Yona anajua kuwa Sara alimsaidia kulea na kuwasomesha watoto ila hataki kumwambia hivyo kwa kuwa anadhani angejishaua.*

*(viii) Elimu ya msichana kutotiliwa maanani. Sara anasema kuwa, wakati wao elimu ya wasichana ilifanyiwa bezo.*

*(ix) Sara anasema kuwa iwapo Yona angeenda kuteka maji kisimani angesemwa na wanakijiji kuwa, amewasomesha watoto ambao wamemweka mama yao mjini na kumwacha baba yao ataabike.*

*(x) Bunju anaona kama kwamba Neema alikuwa ameunda serikali ndani ya nyumba uyake Bunju. Hii ni kwa kuwa, Neema alikuwa nje kazini mara nyingi na angemwachia majukumu kama vile kumsadia Lemi kufanya kazi ya shuleni.*

*(xi) Sara hakusoma sana kwa kuwa siku zao* ***msichana alipobaleghe alikuwa akishinikizwa hadi aolewe****.*

*(xii)* *Kulingana na Luka, zamani* ***mila zao hazikuruhusu watoto wa kike kwenda skuli*** *au kurithi mali.*

*(xiii)* *Kwa maoni ya Beni,* ***mume ambaye ni mwanamume kamili hangoji kuelezwa kuhusu kinachofanyika*** *bali hushirikishwa katika hicho kinachofanywa.*

*(xiv)* *Sara anamwambia Neema kuwa Yona alimsaidia kwa kazi ila anafanya* ***inapobidi au anapojisikia tu****.*

*(xv)* *Utamaduni kuchukuliwa kuwa,* ***hekima ya mwanamke si hekima****. Katika jamii ya kina Sara hekima haikuwa hekima iwapo ilitoka kwa mwanamke.*

(b)-Kukosa watoto-*Sara na Yona walikaa muda mrefu kabla kujaliwa watoto katika ndoa yao.*

-Mapigo katika ndoa-*Sara alipokea kichapo cha mbwa kutoka kwa mumewe Yona alipokuwa mlevi*

-Kusemwa na watu-*Watu waliwasema sana Yona na Sara kwa kukosa watoto na hata baada ya kupata watoto wa kike wanawasema kwa kukosa mrithi wa ardhi ya Yona*

*-Ndoa kama asasi iliyojaa bughudha - Asna anaona ndoa ya Neema, dadake kama iliyojaa matatizo yasiyoweza kuvumilka. Bunju anaonwa kama mchoyo na asiyetaka kumsaidia mtu*

*-Mahitaji ya familia ya upande mmoja katika ndoa kuathiri uhusiano katika ndoa. Neema anahitaji pesa za kumlipia mamake matibabu, pesa ambazo Bunju haridhii kumpa. hHali hii inazua kutoelewana*

*-Ndoa kuingiliwa na watu wa nje. Yoana anashauriwa kumwoa mke mwingine au apate mtoto nje ya ndoa ili awe na mrithi. Wanaomshauriwa ni watu nje ya ndoa*

-Kuwepo kwa taasubi ya kiume-*Awali Yona hakuingia jikoni kumsaidia mkewe katika upishi alipokuwa mgonjwa kwa kuwa alikuwa mwanamume*

-Ugomvi katika ndoa-*Neema na Bunju wanakosa kuelewana kuhusu matokeo ya Lemi ya shuleni.*

-Maradhi-*Sara anaugua ugonjwa wa moyo uliosababishwa na mapigo ya Yona.*

-Kuozwa mapema-S*ara anasema kuwa mtoto as kike aliozwa mapema hivyo hangeweza kuendelea na elimu yake.*

Zozote 9 x 1 = 9

***<u>MWONGOZO-HADITHI FUPI</u>***

6. **Yussuf Shoka Hamad**: "***Mzimu wa Kipwerere!"***

a) Muktadha wa dondoo (alama 4)

i. **Haya ni maneno ya Salihina**
ii. **Salihina anamwambia Bishoo**
iii. **Ni katika Mzimu wa Kipwerere**

**Anataka kujua kuhusu usambazaji wa dawa za kulevya**

**(zozote 4×1=04)**

b) Mbinu za kimtindo katika dondoo. (alama 3)

i. **Jazanda – mzigo kumaanisha dawa za kulevya**
ii. **Nidaa / siyahi – hauuzwi kwa wingi!**
iii. **Swali la balagha - Vipi kuhusu usambazaji wa mizigo? / Umelifikiriaje hili?**

**(za kwanza 3×1=03)**

c) Msemaji ni Salihina (alama 5)

i. **Ni mwadilifu – anapata nafasi ya kuongoza Mzimu kwa sababu ya uadilifu wake.**
ii. **Ni mtamaduni – yeye ndiye anayetenda shughuli za kimila kama vile matambiko katika Mzimu wa Kipwerere**
iii. **Ni mzinifu – anazini na Bishoo ambaye ni mke wa mtu**
iv. **Ni mwenye siri - hatoi sri kwa watu wengine kuwa msitu huu hauna mashetani**
v. **Ni karimu – anamkaribisha Bishoo kwa vileo katika Mzimu wa Kipwerere**
vi. **Ni mnafiki – anasambaza miadarati kupitia Mzimu wa Kipwerere ilali yeye ndiye kiongozi anayeaminika kuwa mwadilifu.**

**(za kwanza 6×1=06)**

d) Suala la dawa za kulevya katika hadithi, "***Mzimu wa Kipwerere***." (alama 7)

i. **Kuna watu kama vile Salihina wanaotumia dawa za kulevya k.v bangi, pombe, sigara na tumbaku katika Mzimu wa Kipwerere.**
ii. **Bishoo anataka kuwatafuta wanawake wengine ili kufanikisha shughuli za kuuza dawa kulevya.**
iii. **Viongozi wanofaa kuuzuia uozo huu ndio wanaouendeleza zaidi – dawa za kulevya ni marufuku ila Salihina ambaye ndiye kiongozi anayeziuza dawa hizi.**
iv. **Wanaoendeleza biashara ya dawa za kulevya huona kazi hizo kama takatifu ilhali ni kinyume na sheria – Salihina anairejelea kama kazi takatifu**
v. **Wanaosambaza dawa hizi wanatumia ujanja ili wasikamatwe – Bishoo anaeleza kuwa watatumia ndoo za kubeba maji kusafirisha dawa hizi ili wasishukiwe na yeyote.**
vi. **Watu wanaingilia biashara hii haramu kwa sababu ya hali ngumu ya maisha – Bishoo anasema kuwa atawapata wanawake wengi kwa sababu hali ya maisha ni ngumu na ajira ni adimu.**
vii. **Watu wanatishwa kutotumia mihadarati kumbe ni viongozi kama Salihina wanaosambaza mihadarati hiyo.**

**(zozote 7×1=07)**

7. (a) Onyesha siri ambazo msemaji hakufichua katika hadithi, "***Kifo cha Suluhu***".

i. **Njia alizotumia ili awe mbunge- mkewe anamwambia kuwa anajua njia alizotumia kupata ubunge**
ii. **Mumewe Suluhu kuhusiana kimapenzi na wanawake wengi wakiwemo binti wa chuo kikuu -Abigael**
iii. **Kumpangia hawara mmoja chumba mjini na kuhusiana naye kimapenzi**
iv. **Kulinyakua shamba la mamake Abigael**
v. **Suluhu kumuua Mamake Abigael baada ya kudai kuwa angemchukulia hatua kisheria baada ya kunyakua shamba lake.**
vi. **Sababu ya kutofanya maendeleo kwani alikuwa akitafuta mbinu ya kulipa deni alilokopeshwa na Bwana Ngoma**
vii. **Kufuja pesa za wananchi kwa kulipa wasichana wa chuo kikuu baada ya kulala nao**

**(zozote 7×1=07)**

(b) "Ni wajibu wetu wanawake kutetea maisha yetu na yale ya Watoto wetu." "***Nipe Nafasi"***

i. **Mama Kazili anaposikia kuwa mumewe Moshe ana mke mwingine, anapeleka malalamishi haya kwa wakweze.**
ii. **Mamake Kazili anapoona kuwa mumewe Moshe hashughulikii familia yake, anaamua kufululiza hadi kwa jamaa mmoja wa mumewe ili wanawe wasije wakafa.**
iii. **Msimulizi anasikia usemi wa mmake wanapopanda Mlima wa Maloti kuwa angerudi kufanya kazi kuwakimu na kuwa lazima wale chajio.**
iv. **Wanaume wanamtaka Mamake Kazili arudi kwao Swazilanda kwa kuwakosea heshima – anawakumbuasha kuwa yeyey ni raia halali wa Lesotho kupitia ndoa na hakuna anayeweza kumlazimisha kurudi Swaziland uk 80**
v. **Mamake Kazili anaeleza jinsi wanawake wanavyohiniwa nafasi na wadhifa katika jamii kwa kusingizia Biblia kuwa mwanamke anafaa kuwa mnyenyekevu na kuomba ruhusa kwa kila kitu afanyacho hata kutembelea familia na marafiki zao.**
vi. **Maneno ya Mamake Kazili yanasababisha wanaume kuwa kimya na hwaamini kwamba mwanamke anaweza kusema mambo kama hayo.**
vii. **Mamake Kazili anasema kuwa anataka ajira na anaambiwa kuwa hapaswi kufanya bila ruhusa kutoka kwa mumewe.**
viii. **Mwanamke mmoja kijijini Habelo anamwambia mumewe kuwa ni mzembe kadamnasi na wanaume wanaanza kukutana kuelezana namna mwanamke huyo alivyokosa heshima. uk 79**
ix. **Mamake Kazili analalamika kuwa mumewe Moshe anamtumia pesa kupitia mama mkwe ila pesa hizo hazimfikii**
x. **Mamake Kazili analalamikia matatizo katika ndoa jambo linalowafanya wanaume kumkemea kwamba anaonyesha mfano mbaya kwa wanawake wengine.**
xi. **Mamake Kazili anapata kazi ya ualimu na anaikimu familia yake kwa chakula na masomo bila kibali cha mtu yeyote.**
xii. **Mamake Kazili anachukua msimamo mkali mbele ya wanaume jambo linalowafanya wanawake wazee kuwataka awaombe msamaha.**
xiii. **Mamake Kazili anamlenga Matweba usoni na kumwambia kuwa anawataka wanawake waelewe kuwa waume wanaposhindwa kutekeleza wajibu wao kama viongozi wa familia hawafai kukaa tu bila kuchukua hatua yoyote. Uk 78**

**(zozote 13×1=13)**

8. (a)

- Maigizo ni sanaa ya mazungumzo yanayoambatana na matendo.
- Ni hali ambapo watendaji hutenda na huiga matendo ya watu au viumbe katika jamii.

(1 x 2 = 2)

(b)

- Hutolewa au huigizwa mbele ya hadhira.
- Uigizaji huhitaji uwanja maalum wa kutendea au mandhari.
- Hufangamana na shughuli za kijamii kama vile utambaji wa hadithi na sherehe.

- Sharti kuwe na tendo la kuigizwa.
- Waigizaji huvaa maleba yanayooana na hali wanazoigiza.
- Maigizo huiga hali ya maisha ya jamii kisiasa, kiuchumi na kitamaduni kwa nia ya kuonyesha mafanikio, udhaifu na migogoro katika nyanja za maisha.
- Huwa na muundo mahsusi wa mtiririko wa matukio.
- Yanaweza kuambatana na ngoma pamoja na uimbaji wa nyimbo au ukariri wa tungo za kishairi.
- Hutumia lugha yenye ufundi mkubwa.
- Wakati mwingine hutumia ishara. Zozote (5 x 2 = 10)

(c) **Dhima ya michezo ya watoto**.

- Hukuza kipawa cha uigizaji miongoni mwa watoto.
- Hukuza ubunifu.
- Ni nyenzo ya kukashifu matendo hasi ya watu wazima.
- Hutambulisha na kusawiri falsafa ya jamii kuhusu malezi na majukumu ya wanajamii.
- Huwapa watoto ukakamavu na kuwawezesha kujiamini wakiwa wangali wachanga.
- Hukuza utangamano/ushirikiano/umoja.
- Huimarisha uwezo wa kukumbuka.
- Huwawezesha kupata mikakati au maarifa ya kukabiliana na hali mbalimbali katika maisha.
- Huburudisha.
- Huendeleze utamaduni wa jamii husika.
- Huhifadhi historia ya jamii husika. n.k. Zozote (4 x 2 = 8)